Kumpenda Mungu

Watu wengi hutamani kuonyesha utii kwa Mungu na hivyo kuonekana kuwa wanampenda. Hata hivyo wako wengi wasiojua namna wawezavyo kumpenda Mungu. “Mkinipenda, **mtazishika amri Zangu**.” Yohana 14:15. “Yeye aliye na amri Zangu, **na kuzishika**, yeye ndiye anipendaye.” Yohana 14:21.

Hizo amri za Mungu ni zipi? “Na Mafarisayo waliposikia ya kwamba amewafumba kinywa wale Masadukayo, walifanya shauri pamoja. Mmoja wao, mwana-sheria, akamwuliza, akimjaribu; Mwalimu, katika torati ni amri ipi iliyo kuu? Akamwambia, Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa akili zako zote. Hii ndiyo amri iliyo kuu, tena **ni ya kwanza**. **Na ya pili yafanana nayo**, nayo ni hii, Mpende jirani yako kama nafsi yako. Katika amri hizi mbili hutegemea torati yote na manabii.” Mathayo 22:34-40. Amri hizi ambazo zimewekwa katika **makundi mawili** ndizo zionyeshazo wajibu wa mwanadamu kwa Mungu wake.

Amri hizi zilizo katika makundi mawili ziliandikwa na Mungu mwenyewe kwa chanda Chake katika mbao mbili za mawe, ubao mmoja ukiwa na kundi moja la amri na mwingine kundi lingine. “Hapo BWANA alipokuwa amekwisha kuzungumza na Musa katika mlima wa Sinai, akampa hizo mbao mbili za ushuhuda, mbao mbili za mawe, zilizoandikwa kwa chanda cha Mungu.” Kutoka 31:18. “Akawahubiri agano Lake, alilowaamuru kulitenda, yaani, zile amri kumi; akaziandika juu ya mbao mbili za mawe.” Kumbukumbu la Torati 4:13. Neno lote la Mungu hujumlishwa katika amri hizi kumi.

Hatuna shaka sasa kwamba wakati Yesu akimwambia yule mwana-sheria ampende Mungu na jirani yake alikuwa akimwambia azitende ama kuzishika amri kumi za Mungu alizoziandika katika mbao mbili za mawe. Ubao wa kwanza ukiwa na amri nne za kwanza zinazouelezea uhusiano kati ya Mungu na mwanadamu, yaani, namna ya kumpenda Mungu. Na ubao wa pili ukiwa na amri sita za pili zinazouelezea uhusiano kati ya mwanadamu na mwanadamu mwenzake, yaani, namna ya kumpenda mwanadamu mwenzake.

Zifuatazo ni amri kumi za Mungu kama zilivyoandikwa katika kitabu cha Kutoka 20:3-17.

I

“Usiwe na miungu mingine ila Mimi.” Kutoka 20:3.

II

“Usijifanyie sanamu ya kuchonga, wala mfano wa kitu cho chote kilicho juu mbinguni, wala kilicho chini duniani, wala kilicho majini chini ya dunia. Usivisujudie wala kuvitumikia; kwa kuwa Mimi, BWANA, Mungu wako, ni Mungu mwenye wivu; nawapatiliza wana maovu ya baba zao, hata kizazi cha tatu na cha nne cha wanichukiao, Nami nawarehemu maelfu elfu wanipendao, na kuzishika amri Zangu.” Kutoka 20:4-6.

III

“Usilitaje bure jina la BWANA, Mungu wako, maana BWANA hatamhesabia kuwa hana hatia mtu alitajaye jina Lake bure.” Kutoka 20:7.

IV

“Ikumbuke siku ya Sabato uitakase. Siku sita fanya kazi, utende mambo yako yote; lakini

siku ya saba ni Sabato ya BWANA, Mungu wako, siku hiyo usifanye kazi yo yote, wewe, wala mwana wako, wala binti yako, wala mtumwa wako, wala mjakazi wako, wala mnyama wako wa kufuga, wala mgeni aliye ndani ya malango yako. Maana, kwa siku sita BWANA alifanya mbingu, na nchi, na bahari, na vyote vilivyomo, akastarehe siku ya saba; kwa hiyo BWANA akaibarikia siku ya Sabato akaitakasa." Kutoka 20:8-11.

V

"Waheshimu baba yako na mama yako; siku zako zipate kuwa nyingi katika nchi upewayo na BWANA, Mungu wako." Kutoka 20:12.

VI

"Usiue." Kutoka 20:13.

VII

"Usizini." Kutoka 20:14.

VIII

"Usiibe." Kutoka 20:15.

IX

"Usimshuhudie jirani yako uongo." Kutoka 20:16.

X

"Usiitamani nyumba ya jirani yako, usimtamani mke wa jirani yako; wala mtumwa wake, wala mjakazi wake, wala ng'ombe wake, wala punda wake, wala cho chote alicho nacho jirani yako." Kutoka 20:17.

Baada ya kuziona hizo amri kumi za Mungu alizokabidhiwa nabii Musa katika mlima wa Sinai, sasa na tujifunze namna ya kuzitenda tukianza na kundi la pili la amri hizo ambazo ziliandikwa katika ubao ule wa pili, zinazouelezea uhusiano kati ya mwanadamu na mwanadamu mwenzake. Ni dhahiri kwamba amri hizi sita hujulikana kwa wanadamu wote duniani kote, kwani ndizo wanadamu huzitumia **kuupima utu, uungwana ama uadilifu wa mtu**. Amri hizi hufundishwa na kuhimizwa na mamlaka zote duniani kwa watu wa tabaka zote. Vitabu vyote vya sheria duniani huzifafanua ama kuzitafsiri tu amri hizi sita ili kuhakikisha haki, usawa, amani, na usalama miongoni mwa wanadamu wote. Uvunjaji wa amri hizi ni jambo lisilokubalika katika jamii yo yote ya binadamu. Na wale wanaozivunja huitwa wahalifu na hukabiliwa na adhabu kama yamkini hata adhabu ya kifo. "Msiwiwe na mtu cho chote, isipokuwa kupendana; kwa maana ampendaye mwenzake ameitimiza sheria. Maana kule kusema, Usizini, Usiue, Usiibe, Usitamani; na ikiwapo amri nyingine yo yote, inajumlishwa katika neno hili, ya kwamba, Mpende jirani yako kama nafsi yako. Pendo halimfanyii jirani neno baya; basi pendo ndilo utimilifu wa sheria." Warumi 13:8-10.

Hivyo basi hizo amri nne zilizotajwa hapo juu na nyingine mbili ambazo hazikutajwa, yaani, ile ya tano, isemayo, "Waheshimu baba yako na mama yako; siku zako zipate kuwa nyingi katika nchi upewayo na BWANA, Mungu wako," na ile ya tisa isemayo, "Usimshuhudie jirani yako uongo," hujumlishwa katika neno, Mpende jirani yako kama nafsi yako. Ni jambo la hakika kwamba **tunaitimiza sheria kwa kuonyesha upendo. Tunatenda dhambi tunapoivunja sheria**.

Wengine wamekuwa wakidhani kwamba amri kumi za Mungu zimepitwa na wakati. Yesu kwa kuliona hili anawaonya wanafunzi Wake, akisema, “Msidhani ya kuwa nalikuja kuitangua torati au manabii; la, sikuja kutangua, bali kutimiliza. Kwa maana, amin, nawaambia, Mpaka mbingu na nchi zitakapoondoka, yodi moja wala nukta moja ya torati haitaondoka, hata yote yatimie.” Mathayo 5:17-18. Hii ni kwa sababu “Katika amri hizi mbili **hutegemea torati yote na manabii**.” Mathayo 22:40. Jambo muhimu na la kuzingatia hapa ni kwamba, torati na maagizo yote ambayo Mungu aliyatoa kupitia manabii Wake, msingi wake ulikuwa ni amri Zake kumi. Kupitia torati na manabii Mungu alikusudia kuzilinda amri Zake.

Jambo lingine muhimu hapa na la kuzingatia ni namna ambavyo Yesu aliitimiliza torati na manabii. “Mmesikia watu wa kale walivyoambiwa, Usiue, na mtu akiua, itampasa hukumu. Bali Mimi nawaambieni, Kila amwoneaye ndugu yake hasira itampasa hukumu.” Mathayo 5:21. “Mmesikia kwamba imenenwa, Usizini; lakini Mimi nawaambia, Kila mtu atazamaye mwanamke kwa kumtamani, amekwisha kuzini naye moyoni mwake.” Mathayo 5:27-28. Tumepata kuelewa sasa ya kwamba kuzivunja amri za Mungu kwaweza kuwa kimwili, yaani, kutenda kwa kutumia viungo vya mwili ama kiroho, yaani, kuwaza au kudhamiria kutenda moyoni. Yesu aliitimiza sheria kwa kuwafundisha wanafunzi Wake namna iwapasavyo kuishika. Hata hivyo hakuruhusu kuzivunja amri kimwili ama kiroho.

Sasa na tuangalie kundi lingine la amri ambalo ndilo la kwanza lijumlishalo amri nne zilizoandikwa katika ubao wa kwanza, zinazouelezea uhusiano kati ya Mungu na mwanadamu, ambazo Yesu anazizungumzia akimwambia mwana-sheria, “Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa akili zako zote. Hii ndiyo amri iliyo kuu, tena ni ya kwanza.” Mathayo 22:37-38. Amri hizi nne za kwanza hazihimizwi wala namna ya kuzishika hakufundishwi na mamlaka mbalimbali duniani kama ilivyo kwa amri sita za pili.

Na tujifunze sasa juu ya amri moja baada ya nyingine miongoni mwa zile amri nne zilizoandikwa katika ubao wa kwanza ambazo Yesu anasema, ni “amri iliyo kuu, tena ni ya kwanza.” Mathayo 22:38.

“Usiwe na miungu mingine ila Mimi.” Kutoka 20:3. Hii ni amri ya kwanza. Mungu anatutaka tumsujudie na kumwabudu Yeye peke Yake. Yesu alipokuwa akijaribiwa na mjaribu, alikataa kumsujudia na kumwabudu. Ibilisi alimtaka Yesu aivunje amri ya kwanza ya Mungu, hata hivyo hakufanikiwa. “Kisha Ibilisi akamchukua mpaka mlima mrefu mno, akamwonyesha milki zote za ulimwengu, na fahari yake, akamwambia, Haya yote nitakupa, ukianguka kunisujudia. Ndipo Yesu alipomwambia, Nenda zako, Shetani; kwa maana imeandikwa, Msujudie Bwana Mungu wako, umwabudu Yeye peke Yake.” Mathayo 4:8-10. Jambo muhimu tunalojifunza hapa ni kwamba, kutoa ibada kwa miungu mingine ama kwa kushiriki katika **ushirikina** au **ukafiri** mwingine uwao wote ili kupata upendeleo fulani na hatimaye kukidhi haja ya moyo ni dhambi mbele za Mungu.

“Usijifanyie sanamu ya kuchonga, wala mfano wa kitu cho chote kilicho juu mbinguni, wala kilicho chini duniani, wala kilicho majini chini ya dunia. Usivisujudie wala kuvitumikia; kwa kuwa Mimi, BWANA, Mungu Wako, ni Mungu mwenye wivu; nawapatiliza wana maovu ya baba zao, hata kizazi cha tatu na cha nne cha wanichukiao, Nami nawarehemu maelfu elfu wanipendao na kuzishika amri Zangu.” Kutoka 20:4-6. Hii ni amri ya pili. Nabii Musa anaendelea kuwatahadharisha wana wa Israeli juu ya amri hii akiwaambia, “Akawahubiri agano Lake, alilowaamuru kulitenda, **yaani,**

zile amri kumi; akaziandika juu ya mbao mbili za mawe. BWANA akaniamuru wakati ule niwafundishe maagizo na hukumu, mpate kuzitenda katika nchi ile mtakayoivukia ili kuimiliki. Jihadharini nafsi zenu basi; maana hamkuona umbo la namna yo yote siku ile BWANA aliyosema nanyi kutoka kati ya moto; msije mkajiharibu nafsi zenu, mkajifanyia sanamu ya kuchonga, mfano wa sura yo yote, mfano wa mwanamume au mwanamke, mfano wa mnyama ye yote aliye duniani, au mfano wa ndege ye yote arukaye mbinguni, au mfano wa kitu cho chote kitambaacho juu ya ardhi, au mfano wa samaki ye yote aliye majini chini ya nchi; tena usije ukainua macho yako hata mbinguni, na ulionapo jua, na mwezi, na nyota, jeshi la mbinguni lote pia, ukashawishwa na kuviabudu, na kuvitumikia, ambavyo BWANA, Mungu wako amewagawanyia watu wote chini ya mbingu zote." Kumbukumbu la Torati 4:13-19.

Ni dhambi kujifanyia mfano wa kitu cho chote chenye uhai au kisicho na uhai, kilicho mbinguni, duniani, au majini chini ya dunia na kukisujudia ama kukiabudu, na kukitumikia. Wapo wengine ambao "Sanamu zao ni fedha na dhahabu, Kazi ya mikono ya wanadamu. Zina vinywa lakini hazisemi, Zina macho lakini hazioni, Zina masikio lakini hazisikii, Zina pua lakini hazisikii harufu, Mikono lakini hazishiki, miguu lakini haziendi, Wala hazitoi sauti kwa koo zake. Wazifanyao watafanana nazo, Kila mmoja anayezitumainia." Zaburi 115:4-8. "Sanamu ya **kuchora** yafaa nini, hata yeye aliyeifanya ameichora? Sanamu ya **kuyeyuka**, nayo ni mwalimu wa uongo, yafaa nini, hata yeye aliyeifanya aiwekee tumaini lake, na kufanya sanamu zisizoweza kusema?" Habakuki 2:18. "Na alaaniwe mtu afanyaye sanamu ya **kuchonga**, au ya **kusubu**, machukizo kwa BWANA, kazi ya mikono ya fundi." Kumbukumbu la Torati 27:15. Sanamu yaweza kuwa ya kuchonga, ya kuchora, ya kuyeyuka au kusubu, zote ni machukizo kwa Mungu. "Paulo alipokuwa akiwangojea huko Athene na kuona jinsi mji ule ulivyojaa sanamu, roho yake ilichukizwa sana ndani yake." Matendo 17:16. Mitume pia walichukizwa na sanamu.

"Usilitaje bure jina la BWANA, Mungu wako, maana Bwana hatamhesabia kuwa hana hatia mtu alitajaye jina Lake bure." Kutoka 20:7. Hii ni amri ya tatu. Kulitumia jina la Bwana kwa namna yo yote isiyo na staha na isiyomrudishia Mungu adhama ni sawa na kulitaja bure jina Lake, hii ni hatia mbele Zake. "Msiape uongo kwa jina Langu, hata ukalinajisi jina la Mungu wako; Mimi ndimi BWANA." Mambo ya Walawi 19:12. Kuapa uongo pia kwa jina la Bwana ni kulitaja bure kusababishako kulinajisi. Jina la Bwana yapasa litajwe wakati tukimsifu na kumwabudu tena kwa kuogopa na kutetemeka, kwani limetukuka mno.

"Ikumbuke siku ya Sabato uitakase. Siku sita fanya kazi, utende mambo yako yote; lakini siku ya saba ni Sabato ya BWANA, Mungu wako, siku hiyo usifanye kazi yo yote, wewe, wala mwana wako, wala binti yako, wala mtumwa wako, wala mjakazi wako, wala mnyama wako wa kufuga, wala mgeni aliye ndani ya malango yako. Maana, kwa siku sita BWANA alifanya mbingu, na nchi, na bahari, na vyote vilivyomo, akastarehe siku ya saba; kwa hiyo BWANA akaibarikia siku ya Sabato akaitakasa." Kutoka 20:8-11. Hii ni amri ya nne.

Je, Sabato ni siku gani? Mtu aweza kutenga siku yo yote katika juma na kuifanya sabato yake? "Na siku ile ilikuwa siku ya Maandalio, na Sabato ikaanza kuingia. Na wale wanawake waliokuja naye toka Galilaya walifuata, wakaliona kaburi, na jinsi mwili Wake ulivyowekwa. Wakarudi, wakafanya tayari manukato na marhamu. **Na siku ya Sabato walistarehe kama**

ilivyoamriwa." Luka 23:54-56. Hapa tunaona siku mbili, siku ya **Maandalio** ambayo wanawake wale walikwenda kuliona kaburi la Bwana wao Yesu Kristo na jinsi mwili Wake ulivyowekwa, na siku ya **Sabato** iliyoanza kuingia baada ya siku ya Maandalio ambayo wanawake hao walistarehe kama ilivyoamriwa. "Hata siku ya kwanza ya juma, ilipoanza kupambazuka, walikwenda kaburini, wakiyaleta manukato waliyoweka tayari. Wakalikuta lile jiwe limevingirishwa mbali na kaburi. Wakaingia, wasiuone mwili wa Bwana Yesu." Luka 24:1-3.

Kutokana na Maandiko hayo, tunaelewa kuwa siku ya Maandalio wanawake walienda kaburini, na siku iyo hiyo waliporudi waliyaweka tayari manukato, lakini siku iliyofuata ambayo ni Sabato walistarehe. Na alfajiri na mapema ya siku ya kwanza ya juma, walikwenda kaburini na manukato yao, wakakuta Bwana Yesu amefufuka. Kote ulimwenguni inajulikana kuwa Bwana Yesu alifufuka Jumapili ambayo ndiyo siku ya kwanza ya juma. Ikiwa Jumapili ni siku ya kwanza ya juma, Jumatatu ni siku ya pili, Jumanne ya tatu, Jumatano ya nne, Alhamisi ya tano, Ijumaa ya sita, na Jumamosi ya saba. Tumeelewa sasa kwamba siku ya Maandalio ni Ijumaa, siku ya Sabato ni Jumamosi, na siku ya kwanza ya juma ni Jumapili. "Siku ya saba ni Sabato ya BWANA, Mungu wako." Kutoka 20:10. Mwanadamu kuwa na siku yake nyingine ya ibada na kuifanya sabato yake badala ya Sabato takatifu ya Bwana ni machukizo mbele Zake, kwani anasema, "Basi mtaishika hiyo Sabato; kwa kuwa ni takatifu kwenu." Kutoka 31:14. **Hakuna siku nyingine katika juma iliyo takatifu isipokuwa Sabato, yaani, siku ya saba ya juma—Jumamosi**. "Kwa ajili ya hayo wana wa Israeli wataishika Sabato, kuiangalia sana hiyo Sabato katika vizazi vyao vyote, ni agano la milele." Kutoka 31:16. Sabato ni agano la milele kati ya Mungu na watu Wake.

Sabato huanza wakati gani? "Mungu akaiita nuru Mchana, na giza akaliita Usiku." Mwanzo 1:5. Siku hufanywa na nuru iitwayo Mchana, na giza liitwalo Usiku. Mchana hutawaliwa na nuru ambayo huonekana pale jua linapoangaza nuru yake, yaani, kunapopambazuka ama kucha, na Usiku hutawaliwa na giza ambalo huonekana pale jua linapoacha kuangaza nuru yake, yaani, linapozama ama kuchwa. **Siku huanza jioni pale jua linapozama na kuisha jioni kesho yake pale jua linapozama tena**. Siku moja inapoisha ndipo siku nyingine huanza papo hapo. "Ikawa jioni ikawa asubuhi, siku moja." Mwanzo 1:5. Neno **ikawa jioni** huonyesha kuwa siku huanza jioni, na ikawa asubuhi huonyesha kuanza kwa sehemu nyingine ya siku hiyo kwani siku moja ina sehemu mbili, yaani, mchana na usiku. Pana tofauti ya majira na nyakati katika sehemu mbalimbali za dunia kutokana na sababu za kijiografia. Hivyo basi, utaratibu huu wa kuanza kuhesabu siku pale jua linapozama ni wa Mungu na ni thabiti.

"Hata ikiisha kuwa jioni, kwa sababu ni Maandalio, ndiyo siku iliyo kabla ya Sabato." Marko 15:42. "Na siku ile ilikuwa siku ya Maandalio, na Sabato ikaanza kuingia." Luka 23:54. Siku ambayo Yesu alisulibiwa msalabani ilikuwa siku ya Maandalio na baadaye katika siku iyo hiyo Sabato ikaanza kuingia. Ilikuwa ni jioni ya siku hiyo ya Ijumaa ambapo Sabato iliingia. **Hivyo basi Sabato huanza Ijumaa jua linapozama na kuisha kesho yake, yaani, Jumamosi jua linapozama**.

Kwa nini Mungu anasema Ikumbuke siku ya Sabato? Kwa sababu ni "Sabato ya BWANA, Mungu wako." Kutoka 20:10. Kwa sababu ni "takatifu kwa BWANA." Kutoka 31:15. Kwa sababu ni "agano la milele." Kutoka 31:16. Ni siku Yake, siku ya kumbukumbu ya uumbaji alioufanya kwa muda wa siku sita. Je, Yesu pia aliishika Sabato na kuitakasa? "Akaenda Nazareti, hapo alipolelewa; na **siku ya Sabato akaingia katika sinagogi kama ilivyokuwa**

desturi Yake, akasimama ili asome." Luka 4:16. Ni hakika kuwa Yesu pia aliishika Sabato na ndiyo maana kwa ajili ya utakatifu wa siku hii anawaonya mbele wafuasi Wake wakati wa dhiki yao "ambayo haijatokea namna yake tangu mwanzo wa ulimwengu hata sasa." Mathayo 24:21, akisema, "Ombeni, ili kukimbia kwenu kusiwe **wakati wa baridi**, wala **siku ya Sabato**." Mathayo 24:20.

Je, mitume pia waliishika Sabato? "Kisha Paulo na wenziwe wakang'oa nanga wakasafiri kutoka Pafo, wakafika Perge katika Pamfilia. Yohana akawaacha akarejea Yerusalemu. Lakini wao wakatoka Perge, wakapita kati ya nchi, wakafika Antiokia, mji wa Pisidia, wakaingia katika Sinagogi **siku ya Sabato**, wakaketi. Kisha, baada ya kusomwa torati na chuo cha manabii, wakuu wa sinagogi wakatuma mtu kwao, na kuwaambia, Ndugu kama mkiwa na neno la kuwafaa watu hawa, lisemeni. Paulo akasimama, akawapungia mkono, akasema, Enyi waume wa Israeli, nanyi mnaomcha Mungu, sikilizeni." Matendo 13:13-16. Paulo anaendelea kusema, "Ndugu zangu, wana wa ukoo wa Ibrahimu, na hao miongoni mwenu wanaomcha Mungu, kwetu sisi neno la wokovu huu limepelekwa. Kwa maana wakaao Yerusalemu, na wakuu wao, kwa kuwa hawakumjua Yeye, wala maneno ya manabii yanayosomwa kila Sabato, wameyatimiza kwa kumhukumu." Matendo 13:26-27. Ni hakika kwamba mitume nao waliishika Sabato. Watu wa Mungu katika ule mji wa Pisidia waliguswa sana na ujumbe wa Paulo alipokuwa katika ibada pamoja na Barnaba siku ya Sabato. "Na walipokuwa wakitoka, wakawasihi waambiwe maneno haya Sabato ya pili. Sinagogi ilipofumukana, Wayahudi na waongofu watauwa wengi wakashikamana na Paulo na Barnaba; ambao, wakisema nao, wakawatia moyo kudumu katika neema ya Mungu. **Hata Sabato ya pili**, watu wengi, karibu mji wote, wakakusanyika walisikie neno la Mungu." Matendo 13:42-44.

Makedonia pia ambako mitume walikwenda kuhubiri Habari Njema, walidumu kusali siku ya Sabato. "Hata **siku ya Sabato** tukatoka nje ya lango, tukaenda kando ya mto, ambapo tukadhani ya kuwa pana **mahali pa kusali**; tukaketi, tukasema na wanawake waliokutana pale." Matendo 16:13.

Siku ya Sabato ni siku aliyoitenga Mungu Mwenyewe iwe siku ya ibada ambapo wanadamu imewapasa waziache kazi zao zote wamwabudu Yeye. Siku hii yaweza pia kutumika kuyagusa mahitaji ya kimwili na ya kiroho ya wahitaji. "Akaondoka huko, akaingia katika sinagogi lao. Na tazama, yumo mtu mwenye mkono umepooza; wakamwuliza, wakisema, Ni halali kuponya watu siku ya Sabato? **Wapate kumshitaki**. Akawaambia, Ni mtu yupi miongoni mwenu mwenye kondoo mmoja, na yule kondoo ametumbukia shimoni siku ya Sabato, asiyemshika akamwopoa? **Je! Mtu ni bora kuliko kondoo mara ngapi**? Basi ni halali kutenda mema siku ya Sabato. Kisha akamwambia yule mtu, Nyosha mkono wako; akaunyosha, ukapona, ukawa mzima kama wa pili." Mathayo 12:9-13. **Hivyo ni halali kutenda mema siku ya Sabato**.

Je, nabii Yohana aliona nini katika Hekalu la Mungu lililoko mbinguni? "Kisha Hekalu la Mungu lililoko mbinguni likafunguliwa, na sanduku la agano Lake likaonekana ndani ya hekalu Lake." Ufunuo 11:19. Tukumbuke kuwa hekalu la duniani lilikuwa ni mfano wa hekalu la mbinguni. Na ndani ya sanduku la agano mlikuwa na mbao mbili za mawe zilizoandikwa amri kumi za Mungu. "Hamkuwa na kitu ndani ya sanduku, ila zile mbao mbili alizozitia Musa huko Horebu, BWANA alipofanya agano na wana wa Israeli, hapo walipotoka Misri." 2 Mambo ya Nyakati 5:10. "Akawahubiri agano Lake, alilowaamuru kulitenda, yaani, zile amri kumi; akaziandika juu ya mbao mbili za mawe." Kumbukumbu

la Torati 4:13. “Mbao zilizoandikwa pande zote mbili, upande huu na upande huu ziliandikwa.” Kutoka 32:15. Ni dhahiri kwamba tutazishika amri za Mungu sio tu katika ulimwengu wa duniani bali hata katika ulimwengu wa mbinguni.

Kama Sabato ya siku ya saba ya juma ni Jumamosi, kwa nini hivi leo watu wengi wanasali Jumapili? Tangu zamani za kale, takriban miaka elfu nne iliyopita, Wapagani walikuwa na mfumo wao wa dini uliojengwa juu ya ibada ya sanamu. Siku yao takatifu ilikuwa ni siku ya kwanza ya juma, ambayo iliitwa siku ya Jua, yaani, Sun-day kwa heshima ya mungu- jua. Hivyo Jumapili iliadhimishwa na wapagani. Hata hivyo katika siku za kutawala kwake Konstantino, mfalme wa Rumi, dola ya kipagani iliyokuwa ikitawala dunia wakati huo, alidai kuwa alikuwa ameongoka na kuwa Mkristo. Ili kujipatia uwezo zaidi, akazikubali desturi nyingi za ibada ya jua kutoka kwa wapagani wale. Nyingine kati ya desturi hizo ni uadhimishaji wa Jumapili. Ilionekana kuwa inafaa zaidi kuwaruhusu wapagani kuitunza siku yao wenyewe ya ibada katika siku ile ya Jumapili, na kuwaomba Wakristo kuungana nao katika kuitunza. Hivyo Konstantino ndiye aliyetoa amri ya kwanza mnamo mwaka wa 321 B.K. ya kuitunza Jumapili badala ya Sabato. Mnamo mwaka wa 330 B.K., Konstantino alihamisha makao makuu ya dola kutoka Rumi kwenda Konstantinopo na kuukabidhi mji wote wa Rumi kwa askofu wa Rumi kuwa kiti chake cha enzi cha Makaisari. Na mnamo mwaka wa 336 B.K., Kanisa Katoliki, katika Baraza la Laodikia lilihamisha utaratibu wa ibada kutoka Jumamosi kwenda Jumapili. Kanisa Katoliki halikuishia hapo tu, mnamo mwaka wa 364 B.K., liliifanya Jumapili kuwa siku takatifu. Kwa kuwa dola ya Rumi ndiyo iliyokuwa ikitawala dunia wakati huo, ijapokuwa iligawanyika mnamo mwaka wa 476 B.K., hata hivyo upapa umeiimarisha amri hiyo ya Konstantino ya kuabudu Jumapili hata kuotesha mizizi kabisa katika Ukristo na Ulimwengu kwa ujumla.

Je, kuna wakati ambapo watu wote duniani watatakiwa kuabudu siku moja? Ni siku ipi hiyo? Ndiyo! Kuna wakati ambapo watu wote duniani watatakiwa kuabudu siku moja. Ni siku ya Jumapili, siku ya kwanza ya juma. Tangazo la kuabudu siku ya Jumapili kitaifa litatolewa katika nchi ya Marekani, nchi iliyo kielelezo cha uhuru wa dini duniani, pale itakapoyaacha madai ya katiba yake yanayoruhusu uhuru wa dini. Sababu kuu ya tangazo hilo itakuwa ni kuokoa uchumi wa nchi hiyo kwa kuongeza siku za kufanya kazi kwa kuwataka wananchi wa nchi hiyo wafanye kazi kwa siku sita katika juma na kupumzika Jumapili badala ya Jumamosi. Ni dhahiri kuwa Marekani ndilo taifa lenye uchumi mkubwa zaidi duniani, hivyo mataifa mengine pia yatashawishika kuiga mfano wa taifa hili ili kuokoa uchumi wa dunia. Hata hivyo wakati huo dunia itakuwa imechanganyikiwa kwa maradhi, vita na njaa. Neno la Mungu linaonya kwamba, ye yote atakayeishika Jumapili “atakunywa katika mvinyo ya ghadhabu ya Mungu iliyotengenezwa, pasipo kuchanganywa na maji, katika kikombe cha hasira Yake; naye atateswa kwa moto na kiberiti mbele ya malaika watakatifu, na mbele za Mwana-Kondoo.” Ufunuo 14:10. “Heri wafu wafao katika Bwana tangu sasa. Naam, asema Roho, wapate kupumzika baada ya taabu zao; kwa kuwa matendo yao yafuatana nao.” Ufunuo 14:13.

Je, tutaokolewa kwa neema? Naam! Ni hakika kwamba tumekwisha kuokolewa kwa neema. “Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani; ambayo hiyo haikutokana na nafsi zenu, ni kipawa cha Mungu.” Waefeso 2:8. Hakuna awezaye kudai kuwa ni kwa uwezo wake yeye mwenyewe anayo haki ya kuokolewa. Ni kwa neema tu ambayo Yesu aliionyesha msalabani Kalvari kwa kuyatoa maisha Yake kwa ajili ya mwanadamu mwenye dhambi ndiyo iwezayo kutuokoa, wala si kwa kujihesabia haki sisi wenyewe kwa matendo ya sheria kama

kwa Mafarisayo. **Wajibu wa mwanadamu ni kumpenda Muumba wake kwa kuzishika amri Zake**. “Na kama siku hizo zisingalifupizwa, asingeokoka mtu ye yote; lakini **kwa ajili ya wateule, zitafupizwa siku hizo**.” Mathayo 24:22. Neema ya Mungu ingalipo na itadumu hata katika wakati ule ambapo watu wa Mungu katika dhiki yao watatafutwa na watesi wao ili wauawe. “**Hapa ndipo penye subira ya watakatifu, hao wazishikao amri za Mungu, na imani ya Yesu**.” Ufunuo 14:12. Wakati huo watu wa Mungu watalazimika kuwa na subira na kudumu kumtumainia Yeye kwamba atawaokoa.

Je, mtu anaweza kushika baadhi tu ya amri miongoni mwa zile kumi na bado akahesabika kuwa anampenda Mungu? La! “Maana mtu awaye yote atakayeishika sheria yote, ila akajikwaa katika neno moja, amekosa juu ya yote. Kwa maana **Yeye aliyesema**, Usizini, pia alisema Usiue. Basi ijapokuwa hukuzini, lakini umeua, umekuwa mvunja sheria.” Yakobo 2:10-11. Ni wazi kwamba mtu huhesabika kama mvunja sheria mbele za Mungu kwa kuivunja hata amri moja tu kati ya zile kumi.

Je, mtu aweza kuwa na imani tu pasipo matendo kisha akahesabiwa haki? “Ndugu zangu, yafaa nini, mtu akisema ya kwamba anayo imani, lakini hana matendo? Je! Ile imani yaweza kumwokoa? Ikiwa ndugu mwanamume au ndugu mwanamke yu uchi na kupungukiwa na riziki, na mtu wa kwenu akawaambia, Enendeni zenu kwa amani, mkaote moto na kushiba, lakini asiwape mahitaji ya mwili, yafaa nini? Vivyo hivyo na imani, isipokuwa ina matendo, imekufa nafsini mwake. Lakini mtu atasema, Wewe unayo imani, nami ninayo matendo. Nionyeshe imani yako pasipo matendo, nami nitakuonyesha imani yangu kwa njia ya matendo yangu. Wewe waamini ya kuwa Mungu ni mmoja; watenda vema. Mashetani nao waamini na kutetemeka. Lakini wataka kujua, wewe mwanadamu usiye kitu, kwamba imani pasipo matendo haizai? Je! Baba yetu Ibrahimu hakuhesabiwa kuwa ana haki kwa matendo, hapo alipomtoa Isaka mwanawe juu ya madhabahu? Waona kwamba imani ilitenda kazi pamoja na matendo yake, na ya kwamba imani ile ilikamilishwa kwa njia ya matendo yale. Maandiko yale yakatimizwa yaliyonena, Ibrahimu alimwamini Mungu, ikahesabiwa kwake kuwa ni haki; naye aliitwa rafiki wa Mungu. Mwaona kwamba mwanadamu huhesabiwa kuwa ana haki kwa matendo yake; si kwa imani peke yake.” Yakobo 2:14-24. “Maana kama vile mwili pasipo roho umekufa, vivyo hivyo na imani pasipo matendo imekufa.” Yakobo 2:26. Hivyo basi imani ni lazima iambatane na matendo. Kuzishika amri zote inawezekana maana “Yasiyowezekana kwa wanadamu yawezekana kwa Mungu.” Luka 18:27.

Shindano kati ya wema na ubaya limekuwa likiendelea kwa karne nyingi, na litaendelea kusitawi kwa kadiri mwisho wa wakati unavyokaribia, Mungu akiwa upande wa wema na shetani upande wa ubaya. Chimbuko la uovu wote ni uvunjaji wa amri kumi za Mungu, Mungu akihimiza wanadamu wazishike, wakati shetani kupitia mawakala wake akifundisha kwamba hazina maana na hazifai kushikwa. Pamoja na kwamba amri zote kumi za Mungu zimekuwa ndio msingi wa pambano kuu kati ya wema na ubaya, hata hivyo pambano la mwisho litahusisha zaidi siku ya ibada. Katika pambano hili la mwisho kila mtu lazima atahusika. “Naye awafanya wote, wadogo kwa wakubwa, na matajiri kwa maskini, na walio huru kwa watumwa, watiwe chapa katika mkono wao wa kuume, au katika vipaji vya nyuso zao.” Ufunuo 13:16. Chapa hii sio kitu kinachoonekana kwa macho kitakachotiwa katika mkono wa kuume au katika kipaji cha uso, bali ni **kukubali kuitunza Jumapili badala ya Jumamosi**—Sabato takatifu ya Bwana. Kwa kadiri tunavyoukaribia mwisho wa pambano hili kati ya wema na ubaya, Sabato ikiwa ndilo jambo linaloshindaniwa, hatimaye makundi mawili tu ya waabuduo yataonekana dhahiri. **Kutakuwa na makundi mawili tu, sio zaidi**. Kila mtu

duniani kote atatakiwa kusimama upande mmoja ama mwingine. Upande wa wanaomtii Mungu ama upande wa wanaomtii mwanadamu; upande wa wanaoishika Sabato takatifu ya Bwana ama upande wa wanaoishika Jumapili, iliyofanywa na mwanadamu kuwa siku ya ibada. Hakuna uvuguvugu, hakuna zaidi. Vyombo vilivyo mstari wa mbele katika harakati za kufanikisha suala hili ni pamoja na upapa, Marekani, wafalme wa nchi, wafanya biashara na viongozi wa dini.

Upapa ndio uko mstari wa mbele zaidi katika harakati hizi ukishirikiana na vyombo vingine kama ilivyoainishwa hapo juu. Kwa miaka mingi limekuwa ni suala gumu na lisilowezekana kuziunganisha dini mbalimbali na kuwa kitu kimoja. Suala hili kwa sasa limezaa matunda makubwa. “Amani na salama,” “Mungu wetu ni mmoja,” ni maneno yenye kuhadaa ambayo yamekuwa yakitumika daima ili kuupamba muungano huu. Marekani kama nchi ya Kiprotestanti inaheshimu uhuru wa dini, lakini pale itakapouunga mkono upapa kwa kutunga sheria itakayowalazimisha wananchi wake kuitunza siku ya kwanza ya juma kinyume na dhamiri zao itakuwa imejitenga kabisa mbali na haki. Kwa sasa jitihada za utungaji wa sheria hii hufanywa katika majimbo mbalimbali ya nchi hiyo.

Majukwaa yafanywayo na nchi mbalimbali duniani hujaribu kuweka mipango ya kuokoa uchumi wa dunia. Harakati hizi zitaendelea na hatimaye itaonekana kuwa suluhisho la kudumu ni kuongeza muda wa kufanya kazi. Mabunge katika nchi mbalimbali yatapitisha sheria itakayowataka wananchi kufanya kazi kwa siku sita, yaani, kuanzia Jumatatu hadi Jumamosi, na kupumzika Jumapili. Ingawa katika nchi mbalimbali duniani kupumzika Jumapili bado halijawa suala la kisheria, hata hivyo sehemu kubwa ya wakazi wa dunia siku hizi hupumzika Jumapili, wakiitumia ama kwa mapumziko ya kawaida ama kwa ibada. Vikao vya bunge pia siku hizi hufanyika kwa siku sita katika juma, isipokuwa Jumapili. Sio jambo la kushangaza siku hizi kuona baadhi hata ya ofisi za umma zikifunguliwa siku ya Jumamosi. Wengi wa wafanya biashara pia wamekuwa wakifunga biashara zao Jumapili wakidai kuwa sio siku ya biashara.

Upapa umefanikiwa kwa kiasi kikubwa kuyaunganisha madhehebu ya dini mbalimbali kupitia viongozi wao. Viongozi wa dini wamekuwa wakitumika kama mawakala wa upapa, shetani akiwatumia kugeuza usikivu wa wafuasi wao kutoka katika amri za Mungu. Kile ambacho Maandiko hutangaza kuwa sheria kamilifu iliyo ya uhuru hutafsiriwa kama kongwa la utumwa. Watu wengi huyakubali maelezo ya viongozi wao wa dini yahusuyo Maandiko hata wasiyachunguze wao wenyewe. Hivyo kwa kufanya kazi kupitia viongozi hawa wa dini, shetani anaweza kuwatawala kulingana na mapenzi yake.

Papa ambaye ndiye kiongozi wa dini mwenye ushawishi mkubwa zaidi duniani, anatumia na ataendelea kutumia ushawishi wake dhidi ya viongozi wa dini mbalimbali ili kuleta umoja miongoni mwa dini hizo. Umoja huu hauwezi kufikiwa pasipo kuwa na umoja katika mafundisho. **Tofauti za kidini zitapunguzwa kwa kadiri iwezekanavyo**, viongozi vipofu wa dini wakidai kuwa “Mungu wetu ni mmoja,” na kuwaaminisha hivyo waumini wao. Msemo huo wenye hila ndani yake utatumika daima kama mtego ili kuibatilisha sheria ya Yehova. Kwa kuwashawishi viongozi wa dini hasa zile zisizokuwa za Kikristo, kusudi la kuwa na siku moja ya ibada duniani kote litakuwa limefikiwa. Hivyo wakati Marekani itakapoitangaza Jumapili kuwa siku ya ibada katika nchi hiyo, sehemu kubwa iliyobaki ya dunia haitastaajabu kwani itakuwa imekwisha zoeleka kuwa ni desturi kupumzika siku ya Jumapili badala ya **Jumamosi kama Mungu alivyoagiza**.

Mungu ni mwingi wa rehema na upendo mkuu usiopimika. Kabla ya kuhukumu daima huwa anatoa onyo kwanza ili kumwacha mwanadamu pasipo udhuru uwao wote. Hakika “Atauhukumu ulimwengu kwa haki; atawaamua watu kwa adili.” Zaburi 9:8.

Onyo lenye kuogofya mno kuwahi kutolewa na Mungu kwa jamii ya binadamu halipatikani mahali po pote isipokuwa katika Ufunuo 14:9, 10. Imeandikwa, “Mtu awaye yote akimsujudu huyo mnyama na sanamu yake, na kuipokea chapa katika kipaji cha uso wake, au katika mkono wake, yeye naye **atakunywa katika mvinyo ya ghadhabu ya Mungu iliyotengenezwa**, **pasipo kuchanganywa na maji**, katika kikombe cha hasira Yake; naye atateswa kwa moto na kiberiti mbele ya malaika watakatifu, na mbele za Mwana-Kondoo.” **Mnyama** katika lugha ya unabii kama ilivyotumika hapa huwakilisha mamlaka, milki, dola, nchi, taifa ama ufalme. “Wanyama hao wakubwa walio wanne ni wafalme wanne watakaotokea duniani.” Danieli 7:17. Mnyama huyu anayezungumziwa hapa huwakilisha **upapa**. **Sanamu** ni mbadala wa kitu halisi. Hivyo sanamu yake ni Jumapili—sabato bandia, itakayofanywa na makanisa ya Kiprotestanti pale yatakapolishawishi bunge kuitangaza kama siku ya ibada nchini Marekani kwa mara ya kwanza kabla haijatangazwa duniani kote. **Chapa** au alama ni ishara ya heshima. Hivyo chapa au alama ya huyo mnyama ni **Jumapili**. Hii ndiyo ishara ya heshima kwa mamlaka ya upapa.

Tangu mwaka wa 364 B.K., pale kanisa la Romani Katoliki lilipotangaza kuwa limehamisha utakatifu kutoka Sabato ya siku ya saba ya juma na kwenda Jumapili, siku ya kwanza ya juma, chapa ya mamlaka yake imekuwa ni Jumapili. Madhehebu mengine yanapoitunza siku hii **hutoa heshima** kwa mamlaka ya upapa. Watu wengi duniani wamekuwa wakiitunza Jumapili badala ya Sabato pasipo kujua kwamba wanatoa heshima kwa mamlaka hii ya upapa. Katika **kipaji cha uso** humaanisha moyoni au akilini, “Linda moyo wako kuliko yote uyalindayo; Maana ndiko zitokako chemchemi za uzima.” Mithali 4:23. Katika **mkono** humaanisha utendaji, “Nitanawa mikono yangu kwa kutokuwa na hatia, Na kuizunguka madhabahu Yako, Ee BWANA.” Zaburi 26:6. Tunaelewa sasa kwamba kuipokea chapa katika kipaji cha uso, au katika mkono, ni kuikubali Jumapili kama siku ya ibada ambako kwaweza kudhihirishwa pia kwa kuitakasa kwa kutokufanya kazi. **Kumsujudu huyo mnyama ni kuonyesha utii, kutoa heshima kwa mamlaka ya upapa kwa kuitunza Jumapili badala ya Sabato ya siku ya saba ya juma**. “Imetupasa kumtii Mungu kuliko wanadamu.” Matendo 5:29. Hukumu itakayomshukia mwanadamu mkaidi hufananishwa na mvinyo iliyotengenezwa pasipo kuchanganywa na maji, ni ghadhabu ya hasira ya Mungu isiyokuwa na rehema hata kidogo. Wakati wa rehema ni sasa. Yesu anasema, “Tazama, naja upesi, na ujira Wangu u pamoja Nami, kumlipa kila mtu kama kazi yake ilivyo.” Ufunuo 22:12. Anaendelea kusema, “Mimi ni Alfa na Omega, mwanzo na mwisho, wa kwanza na wa mwisho. Heri wazifuao nguo zao, wawe na amri kuuendea huo mti wa uzima, na kuingia mjini kwa milango yake. Huko nje wako mbwa, na wachawi, na wazinzi, na wauaji, na hao waabuduo sanamu, na kila mtu apendaye uongo na kuufanya.” Ufunuo 22:13-15.

© 2022, na Moses K. Wandwi

+255 686 412 622

+255 718 166 452

mwandwi12@gmail.com